



# NYOSHA MKONO KWA HURUMA

*Unapofuata mfano wa Mwokozi wa huruma, utaona kwamba unaweza kuleta tofauti katika maisha ya wengine.*

**H**uruma ni kuwa na ufahamu wa dhiki ya wengine pamoja na hamu ya kufanya iwe rahisi au kufariji. Agano la kumfuata Mwokozi ni agano la huruma la “kubeba mizigo ya mmoja na ya mwingine” (Mosia 18:8). Kazi ya kuwatunza wengine ni fursa ya kuhudumu kama ambavyo Mwokozi anghudumu kwa “huruma, akileta tofauti” (Yuda 1:22). Bwana aliamuru, “Kila mtu na amwonee ndugu yake rehema na huruma” (Zakaria 7:9).

## **Huruma ya Mwokozi**

Huruma ilikuwa ni kichocheo katika huduma ya Mwokozi (ona maandishi ya pembeni mtandaoni: “Mwokozi Mwenye Huruma”). Huruma Yake kwa mwanadamu mwenzake ilimfanya Yeye kuwafikia wale waliomzunguka kwa nafasi zisizohesabika. Akitambua mahitaji ya watu na hamu zao, Yeye angeweza kuwabariki na kuwafundisha katika njia ambazo zilikuwa na maana zaidi kwao. Hamu ya Mwokozi ya kutuina juu ya dhiki yetu ilipelekea hatimaye kwenye tendo kuu la

huruma: Upatanisho Wake kwa dhambi na mateso ya mwanadamu.

Uwezo Wake wa kuitikia mahitaji ya watu ndicho kitu ambacho tunaweza kujitahidi kukipata tunapohudumu. Tunapoishi kwa haki na kusikiliza miongo wa Roho, tutapata muongozo wa kiungu kunyosha mkono katika njia za maana.

## **Agano Letu la Huruma**

Baba wa Mbinguni anawataka watoto Wake kuwa wenye huruma (ona 1 Wakorintho 12:25–27). Ili kuwa wafuasi wa kweli, lazima tukuze na kuonyesha huruma kwa wengine, hasa kwa wale wenye uhitaji (M&M 52:40).

Kujichukulia juu yetu jina la Yesu Kristo kupitia agano letu la ubatizo, tunashuhudia kwamba tuko radhi kuonyesha huruma. Rais Henry B. Eyring, Mshauri wa Pili katika Urais wa Kwanza, alifundisha kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu hutusaidia kufanya hivyo: “Wewe ni muumini wa agano wa Kanisa la Yesu Kristo.

“Hii ndiyo sababu una mawazo ya kutaka kumsaidia anayetaabika kusonga mbele chini ya mzigo wa huzuni na mateso. Uliahidi kwamba ungesaidia Bwana kufanya mizigo yao iwe miepesi na kufarijiwa. Ulipewa uwezo wa kuwasaidia kupunguza uzito wa mizigo hiyo pale ulipopokea kipawa cha Roho Mtakatifu.”<sup>1</sup>

Kwa mfano, dada huko Russia alikuwa na hali ngumu ya kifamilia ambayo ilimfanya kutohudhuria kanisani kwa zaidi ya mwaka mmoja. Dada mwingine katika tawi alinyoosha mkono kwa huruma kila Jumapili kwa kumpigia simu kumwambia kuhusu mahubiri, masomo, miito ya kwenda misheni, watoto waliozaliwa, na taarifa nyingine za tawi. Wakati hali ya kifamilia ya dada iliyo-mweka ndani ilipotatuliwa, alihisi kana kwamba alikuwa bado sehemu ya tawi kwa sababu ya simu alizopigiwa na rafiki yake kila wiki.

#### MUHTASARI

1. Henry B. Eyring, “Mfariji,” *Liahona*, Mei 2015, 18.

### MAPENDEKEZO MANNE YA KUKUZA HURUMA

Wakati huruma daima huongezeka baada ya kupitia uzoefu wa majaribu yetu wenyewe, kuna baadhi ya mambo tunaweza kufanya leo ili kukuza huruma. Fikiria njia ambazo kwazo ungeweza kutumia kanuni hizi nne:

**Omba ili kuipata.** Unaposihi kwa Baba wa Mbinguni, Yeye atafungua moyo wako, na “utahisi kujali kwa dhati kwa ajili ya ustawi na furaha ya milele ya watu wengine” (*Hubiri Injili Yangu: Muongozo wa Huduma ya Umisionari* [2004], 118; ona pia Moroni 7:48).

**Ifanyie kazi.** Wewe pia unaweza kuonyesha huruma kwa kusikiliza na kuelewa. Jiweke katika hali

yao na fikiria jinsi wanavyoweza kuwa wanahisi. Kama inafaa kwa hali na wakati, unaweza kujitolea kusaidia kutuliza maumivu yao, mateso, au dhiki.

**Fuata minong’ono.** Bwana anaweza kutufunulia njia za kuonyesha huruma ambazo hatukuweza kuzigundua sisi wenyewe. Unapohisi muashirio kutoka kwa Roho wa kuwasaidia wengine, usisite kuufanyia kazi.

**Kuwa rafiki binafsi.** Kuonyesha huruma kunaweza kuwa rahisi kama kuonyesha shauku ya kweli kwenye maisha ya watu. Jifunze kusikiliza vizuri zaidi (ona “Kanuni za Kuhudumu: Vitu Vitano Wasikilizaji Wazuri Huvifanya,” *Liahona*, Juni 2018, 6–9). Upendo wako kwao utaongezeka, na itakuwa rahisi kutambua njia za kuonyesha upendo huo.

### MWOKOZI MWENYE HURUMA

Fikiria kujifunza baadhi ya maandiko haya kuona jinsi huruma ya Yesu Kristo ilivyomsukuma Yeye kuonya, kubariki, na kufundisha wale waliomzunguka wakati wa huduma Yake: Mathayo 9:35–38; 14:14; 18:27, 33; 20:30–34; Marko 1:40–42; 5:19; 6:30–42; 9:22; Luka 7:13; 10:33; 15:20.

Kanuni za kuhudumu zimekusudiwa kutusaidia kujifunza kutunzana sisi kwa sisi—sio kushirikiwa kama ujumbe. Tunapokuja kuwajua wale tunao-wahudumia, Roho Mtakatifu atatushawishi kujua ni ujumbe gani watahitaji kuongezea kwenye ulinzi wetu na huruma.